**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**021** **KISWAHILI**

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3:00** **Jumanne, 31 Oktoba 2017 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi na tano (15)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni lazima.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 10)**
**UFAHAMU**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Mipango ya elimu katika nchi mbalimbali duniani siku zote inahitilafiana, kimuundo na elimu itolewayo. Mipango hiyo huhitilafiana kwa sababu nchi zenyewe zinazotoa elimu huhitalifiana, kwa sababu elimu yoyote iwe ya darasani au si ya darasani, ina shababa yake. Shabaha yenyewe ni kurithishana maarifa na mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine na kuwaandaa vijana wawe tayari kuchukua nafasi zao katika kulitumikia na kuliendeleza taifa. Hivi ndivyo ilivyo katika nchi zote yaani nchi za kikabaila za Magharibi, nchi za kikomunist za Mashariki na hata zilivyokuwa nchi za kiafrika kabla ya ukoloni.

Kwa hiyo, sio kweli kusema kwamba kabla ya ukoloni waafirka hawakuwa na elimu, eti kwa sababu tu hawakuwa na shule, na kwamba makabila machache yalitoa mafunzo kwa muda mfupi tu kambini. Watoto na vijana walijifunza kwa kuishi na kutenda. Nyumbani au shambani walijifunza ufundi wa kazi zilizopaswa kufanywa, pamoja na tabia wanayopaswa kuwa nayo watu wa jamii ile. Vile vile walifijunza aina za majani na mizizi ya miti ya porini, na kazi zake; walijifunza namna ya kushughulikia mavuno na jinsi ya kuangalia mifungo. Haya yote waliyafanya kwa kushirikiana na wale waliowazidi umri au wakubwa kuliko wao.

HIvyo jamii zilijifunza historia za makabila yao, na uhusiano baina ya kabila moja na makabila mengine, uhusiano baina ya makabila yao na mizimu kwa kusikiliza tu hadithi zilizokuwa zikitolewa na wazee. Kwa njia hii na kwa desturi za kushirikiana walizofunzwa vijana, tamaduni za nchi ziliendelezwa. Kwa hiyo elimu waliyopata haikuwa y kukosekana kwa madarasa hakumaanishi kwamba hakukuwako elimu, wala hakukupunguza umuhimu wa elimu katika Taifa. Kwa msingi hiyo inawezekana kabisa kwamba elimu aliyokuwa akiipata kijana wa enzi zile ilikuwa elimu inayomfaa kuishi katika jamii yake.

Huko Ulaya elimu ya darasani ilianza siku nyingi. Lengo la elimu hiyo ya Ulaya ilikuwa sawa na ile iliyotolewa kwa mtindo wa asili wa Kiafrika, yaani, kwa kuishi na kutenda. Madhumuni makubwa yalikuwa ni kuimarisha mila zilizokuwa zikitumika katika nchi, na kuwanadaa awatoto na vijana kutimiza wajibu wao katika nchi hiyo. Na hivyo ndivyo ilivyo katika nchi za kikomunisti siku hizi. mafunzo yanayotolewa ni tofauti na yale yanayotolewa katika nchi za Magharibi, lakini lengo likiwa ni moja; kuwaandaa vijana kuishi katika taifa na kulitumikia taifa hilo, na kuendeleza busara, ujuzi na mila za taifa katika kizazi kijacho. Mahali popote ambapo elimu inashindwa kutimiza malengo hayo, basi maendeleo ya nchi hiyo yatalegalega, vinginevyo kutatokeo malalamiko watu watakapogundua kwamba elimu yao imewaandalia kuishi maisha ambayo kwa kweli hayapo.

**Maswali**

(a) Eleza sababu mbili zinazosababisha nchi mbali mbali kuhitilafiana katika muundo wake wa elimu.
(b) (i) Fafanua namna jamii za kiafrika zilivyokuwa zinatoa elimu kwa watu wake.
(ii) Ni nami waliohusika kutoa elimu katika jamii za kiafrika?
(c) Elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika na ile iliyotolewa huko Ulaya zilikuwa na malengo gani?
(d) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma.


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

2. Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasipungua mia moja (100) na yasiyozidi mia moja na arobaini (140).

**SEHEMU B (Alama 25)**
**SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Katika kila sentensi uliyopewa, orodhesha vishazi huru katika **Safu A** na vishazi tegemezi katika **safu B.**
   (a) Ngoma hailii vizuri kwa kuwa imepasuka.
   (b) Watoto walioandikishwa watakuja kesho.
   (c) Kiongozi atakayefunga mkutano amepelekewa taarifa.
   (d) Mtawatambua walio wasikivu.
   (e) Kitabu ulichopewa kina kurasa nyingi.

4. (a) Eleza maana ya kielezi kwa kutoa mfano wa sentensi moja.
   (b) Kwa kila tungo uliyopewa pigia mstari kielezi na kisha taja ni cha aina gani.
      (i) Darasani kuna utulivu mkubwa
      (ii) Wanafunzi wanaimba kimasihara.
      (iii) Mwalimu amerudi tena.
      (iv) Nitaondoka wiki inayokuja.

5. Toa maana tano tofauti za neno “kibao” kisha tunga sentensi moja kwa kila maana uliyotoa.

6. Moja ya faida ya misimu ni kuhifadhi historia ya jamii. Toa mfano mmoja wa misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi vifuatavyo:
   (a) Muda mfupi baada ya kupata uhuru.
   (b) Miaka ya Azimio la Arusha.
   (c) Njaa ya mwaka 1974/1975.
   (d) Miaka ya vita vya Kagera.
   (e) Kipindi cha hali ngumu ya maisha baada ya vita vya Kagera.

7. (a) Eleza maana ya kiarifu.
   (b) Kwa kutumia mifano, taja miundo minne ya kiarifu.

**SEHEMU C (Alama 10)**
**UANDISHI**
Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Andika barua kwa rafiki yako kuhusu mipango yako ya baadaye utakapoaliza Kidato cha Nne. Jina la rifiki yako liwe Dito Jito wa S.L.P 300 Longido na jina lako liwe Kijito Bahari wa Shule ya Sekondari Mtaweza, S.L.P 200 Dar-es-Salaam.

9. Andika insha ya hoja isiyopungua maneno mia mbili na hamsini (250) na isiyozidi maneno mia tatu (300) kuhusu ‘Madhara ya Madawa ya Kulevya nchini Tanzania’.


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU D (Alama 10)**
**MAENDELEO YA KISWAHILI**
Jibu swali la **kumi (10)**

10. "Lugha ya Kiswahili imetokana na lahaja za Kibantu." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja mbili kuelezea chanzo cha lahaja na hoja tatu kuhusu matumizi ya lahaja katika Kiswahili sanifu.

**SEHEMU E (Alama 45)**
**FASIHI KWA UJUMLA**
Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| **Wasakatonge** | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| **Malenga Wapya** | - | TAKILUKI (DUP) |
| **Mashairi ya Chekacheka** | - | T.A. Mvungi (EP & D.LTD) |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Takadini** | - | Ben J. Hanson (MBS) |
| **Watoto wa Maman'tilie** | - | E. Mbogo (H.P) |
| **Joka la Mdimu** | - | A.J. Safari (H.P) |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Orodha** | - | Steve Reynolds (MA) |
| **Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe** | - | E. Semzaba (ESC) |
| **Kilio Chetu** | - | Medical Aid Foundation (TPH) |

11. Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika maandishi hupoteza uhai na uhalisia wake. Fafanua changamoto nne zinazoweza kujitokeza kwa kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi.

12. "Msanii ni kinda la jamii husika hivyo anayoandika huihusu jamii hiyo." Jadili kauli hii kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma.

13. "Elimu ni ufunguo wa maisha." Fafanua kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kati ya vitabu viwili vya riwaya vilivyoorodheshwa.

14. "Wahusika katika kazi za fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao." Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja tatu kwa kila mhusika kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma.

15. Tunga shairi la kimapokeo lenye beti nne kuhusu "Rafiki yako anayechamia shule nyingine."


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org